**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

# MUHTASARI WA PATO LA TAIFA
# ROBO YA TATU (JULAI – SEPTEMBA) 2022
# BEI ZA MWAKA WA KIZIO 2015

**Ofisi ya Taifa ya Takwimu**
**Wizara ya Fedha na Mipango**
**Desemba 2022**

**Yaliyomo**

Majedwali ........ 4
Orodha ya Vielelezo ........ 5
Viambatisho ........ 6
1.0 Utangulizi ........ 7
1.1 Uchumi wa Dunia ........ 7
1.2 Uchumi wa Nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara ........ 7
1.3 Uchumi wa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ........ 7
1.4 Uchumi wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ........ 8
1.5 Uchumi wa Tanzania ........ 9
1.5.1 Pato la Taifa, Robo ya Tatu Mwaka 2022 ........ 10
1.5.2 Mchango katika Pato la Taifa, Robo ya Tatu Mwaka 2022 ........ 10
1.5.3 Ukuaji wa Shughuli za Uchumi Robo ya Tatu, Mwaka 2022 ........ 11
1.5.4 Mchango katika Kiwango cha Ukuaji Robo ya Tatu, Mwaka 2022 ........ 12
2.1 Ukuaji wa Uchumi kwa Shughuli za Kiuchumi ........ 12
2.2 Kilimo, Misitu na Uvuvi ........ 12
2.2.1 Mazao ........ 12
2.2.2 Mifugo ........ 13
2.2.3 Misitu ........ 14
2.2.4 Uvuvi ........ 14
2.3 Uchimbaji Madini na Mawe ........ 14
2.4 Uzalishaji Viwandani ........ 15
2.5 Umeme ........ 15
2.6 Maji ........ 16
2.7 Ujenzi ........ 16
2.8 Biashara na Matengenezo ........ 17
2.9 Uchukuzi na Uhifadhi wa Mizigo ........ 17
2.10 Huduma ya Malazi na Chakula ........ 18
2.11 Habari na Mawasiliano ........ 18
2.12 Fedha na Bima ........ 18
2.13 Upangishaji Majengo ........ 19
2.14 Shughuli za Kitaalam, Ufundi na Sayansi ........ 20
2.15 Huduma Zinazohusiana na Utawala ........ 20
2.16 Utawala na Ulinzi ........ 20
2.17 Elimu ........ 21
2.18 Afya ........ 21
2.19 Huduma Nyingine za Jamii ........ 21
3.0 Hitimisho ........ 22

## Majedwali

Jedwali Na. 1: Uzalishaji wa Madini, Robo ya Tatu Mwaka 2016 – 2022 ....................................... 15
Jedwali Na. 2: Viashiria vya Huduma za Mawasiliano, Robo ya Tatu Mwaka 2020 – 2022 ........... 18

## Orodha ya Vielelezo

Kielelezo Na. 1: Ukuaji wa Uchumi kwa Baadhi ya Nchi za SADC, Robo ya Tatu Mwaka 2021 na 2022 ........ 8
Kielelezo Na. 2: Ukuaji wa Uchumi kwa Baadhi ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Robo ya Tatu Mwaka 2018 - 2022 ........ 9
Kielelezo Na. 3: Kiwango cha Ukuaji wa Pato la Taifa, Robo ya Tatu Mwaka 2016 – 2022 ........ 10
Kielelezo Na. 4: Mchango katika Pato la Taifa kwa Bei za Miaka Inayohusika ........ 11
Kielelezo Na. 5: Viwango vya Ukuaji wa Shughuli za Uchumi, Robo ya Tatu, Mwaka 2022 ........ 11
Kielelezo Na. 6: Uzalishaji wa Baadhi ya Mazao, Robo ya Tatu Mwaka 2021 na 2022 ........ 13
Kielelezo Na. 7: Jumla ya Mikopo na Amana (Sh. Trilioni), Robo ya Tatu Mwaka 2017 – 2022 ... 19

## Viambatisho

Kiambatisho Na. 1: Pato la Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi kwa Bei za Mwaka 2015 – Sh. Milioni ........ 23
Kiambatisho Na. 2: Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi kwa Bei za mwaka 2015 – Asilimia ........ 25
Kiambatisho Na. 3: Pato la Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi kwa Bei za Soko (Bei za Miaka inayohusika) – Sh. Milioni ........ 27
Kiambatisho Na. 4: Mchango wa Shughuli za Kiuchumi katika Pato la Taifa kwa Bei za Soko (Bei za miaka inayohusika) – Asilimia ........ 29

## 1.0 Utangulizi

Pato la Taifa kwa robo mwaka ni kiashiria chenye taarifa za kina za mwenendo wa uchumi kwa aina ya shughuli za kiuchumi. Kiashiria hiki hutumika katika kutathmini mwenendo wa uchumi kwa vipindi vifupi vifupi kwa lengo la kutunga na kutathmini utekelezaji wa sera za kiuchumi kwa wakati muafaka katika nchi.

## 1.1 Uchumi wa Dunia

Kwa mujibu wa ripoti ya hali ya uchumi wa dunia iliyotolewa na Shirika la Fedha Duniani (IMF) mwezi Oktoba 2022, ilionesha uchumi wa dunia kwa mwaka 2022 ulikadiriwa kukua kwa kiwango cha **asilimia 3.2** sawa na kiwango kilichokuwa kimekadiriwa mwezi Julai 2022. Kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia kumetokana na sababu mbalimbali zikiwemo: Vita kati ya Urusi na Ukraine, kupanda kwa gharama za maisha kutokana na kuendelea kuongezeka kwa mfumuko wa bei, mabadiliko ya tabia nchi na kupungua kwa ukuaji wa uchumi wa Nchi ya China.

## 1.2 Uchumi wa Nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara


Ukuaji wa uchumi wa nchi zilizo kusini mwa Jangwa la Sahara kwa mwaka 2022 ulikadiriwa kukua kwa **asilimia 3.6**. Makadirio hayo, yamepungua kwa pointi za asilimia 0.2 yakilinganishwa na makadirio yaliyotolewa kwenye ripoti ya hali ya uchumi wa dunia ya mwezi Julai 2022. Ripoti ya mwezi Oktoba 2022 inaonesha uchumi wa Nchi ya Afrika Kusini unakadiriwa kukua kwa **asilimia 2.1** mwaka 2022 sawa na upungufu wa pointi 0.2 za asilimia ikilinganishwa na asilimia 2.3 iliyokuwa imekadiriwa kwenye ripoti ya mwezi Julai 2022. Vilevile, makadirio ya mwezi Oktoba 2022, yameonesha kuwa, mwaka 2022 uchumi wa Nigeria unakadiriwa kukua kwa **asilimia 3.2** sawa na upungufu wa pointi za asilimia 0.2 ikilinganishwa na makadirio mwezi Julai 2022.

## 1.3 Uchumi wa Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC)

Kwa mujibu wa ripoti ya Shirika la Fedha Duniani (IMF) ya makadirio ya ukuaji wa uchumi ya mwezi Oktoba 2022, ukuaji wa uchumi katika nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika unatarajiwa kukua kwa **asilimia 3.6** mwaka 2022 ambayo ni sawa na upungufu wa pointi 0.2 za asilimia ikilinganishwa na maoteo yaliyofanyika kwenye ripoti iliyotolewa mwezi Julai 2022.

Ukuaji wa uchumi kwa baadhi ya nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika kama vile Afrika kusini umeongezeka kwa kiwango cha **asilimia 4.1** katika robo ya tatu ya mwaka 2022 ukilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.0 kipindi kama hicho mwaka 2021. Uchumi wa Namibia uliongezeka kwa kiwango cha **asilimia 4.3** katika robo ya tatu mwaka 2022 ukilinganisha na ukuaji wa asilimia 5.6 kipindi kama hicho mwaka 2021. Aidha, uchumi wa Tanzania umeongezeka kwa kiwango cha **asilimia 5.2** katika robo ya tatu mwaka 2022 ukilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.5 kipindi kama hicho mwaka 2021.

**Kielelezo Na. 1: Ukuaji wa Uchumi kwa Baadhi ya Nchi za SADC, Robo ya Tatu Mwaka 2021 na 2022**





Chanzo: Ofisi za Takwimu za Nchi Husika, 2022 (www.statssa.gov.za, www.nsa.org.na, www.nbs.go.tz)

## 1.4 Uchumi wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki

Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ambazo taarifa za mwenendo wa uchumi katika robo ya tatu ya mwaka 2022 zimepatikana kwenye tovuti za taasisi hizo zimeonesha kuendelea kuimarika kwa ukuaji wa uchumi kwa kuendelea kuwa na ukuaji chanya ambapo uchumi wa Nchi ya Rwanda umeongezeka kwa **asilimia 10.0**. ukilinganishwa na asilimia 10.1 kipindi kama hicho mwaka 2021. Uchumi wa Nchi ya Kenya umeongezeka kwa **asilimia 4.7** ukilinganishwa na asilimia 9.3 mwaka 2021; Uchumi wa Nchi ya Uganda umeongezeka hadi **asilimia 7.5** kutoka asilimia 2.7 kipindi kama hicho mwaka 2021. Aidha, uchumi wa Tanzania umekua kwa kiwango cha **asilimia 5.2** ukilinganishwa na asilimia 5.5 mwaka 2021. Nchi nyingine

za Jumuiya ya Afrika Mashariki bado hazijatoa mwenendo wa ukuaji wa uchumi katika kipindi cha mwezi Julai hadi Septemba 2022.

**Kielelezo Na. 2: Ukuaji wa Uchumi kwa Baadhi ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Robo ya Tatu Mwaka 2018 - 2022**




Chanzo: Ofisi za Takwimu za Nchi Husika, 2022 (www.statistics.gov.rw, www.knbs.or.ke, www.ubos.org, www.nbs.go.tz)

## 1.5 Uchumi wa Tanzania

Utayarishaji wa Takwimu za Pato la Taifa robo ya tatu (Julai - Septemba) 2022 umetumia taarifa zilizokusanywa kutoka katika shughuli zote za kiuchumi nchini. Aidha, utayarishaji umezingatia Mwongozo wa Kimataifa wa Kutayarisha Takwimu zaPato la Taifa unaojulikana kama ***2008 System of National Accounts***. Taarifa hii inahusu Pato la Taifa kwa Tanzania Bara kwa bei za mwaka husika na Pato Halisi la Taifa (kwa bei za mwaka wa kizio 2015).

Aidha, Ofisi ya Taifa ya Takwimu inaendelea kutekeleza Sera ya Mapitio ya Takwimu za Pato la Taifa iliyoanza kutumika mwaka 2019 baada ya kukamilisha marekebisho ya Takwimu za Pato la Taifa kwa mujibu wa Mwongozo wa Kimataifa wa Kutayarisha Takwimu za Pato loa Taifa. Sera hii inaruhusu kuchapisha matokeo ambayo yanaweza kufanyiwa mapitio kutokana na kupatikana kwa takwimu mpya au zilizofanyiwa mapitio za kila robo mwaka na za kila mwaka.

### 1.5.1 Pato la Taifa, Robo ya Tatu Mwaka 2022

Katika robo ya tatu ya mwaka 2022, Pato la Taifa kwa bei za mwaka husika liliongezeka hadi Shilingi Trilioni 42.9 kutoka Shilingi Trilioni 38.4 kipindi kama hicho mwaka 2021. Aidha, Pato Halisi la Taifa (kwa bei za mwaka wa kizio 2015) liliongezeka hadi Shilingi Trilioni 33.9 katika robo ya tatu mwaka 2022 kutoka Shilingi Trilioni 32.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2021, sawa na **ukuaji wa asilimia 5.2**.

**Kielelezo Na. 3: Kiwango cha Ukuaji wa Pato la Taifa, Robo ya Tatu Mwaka 2016 – 2022**





Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2022

### 1.5.2 Mchango katika Pato la Taifa, Robo ya Tatu Mwaka 2022

Mchanganuo wa mchango katika Pato la Taifa kwa shughuli kuu za kiuchumi katika robo ya tatu ya mwaka 2022 unaonesha kuwa: Shughuli za Huduma (Biashara na Matengenezo; Malazi na Chakula; Uchukuzi na Uhifadhi Mizigo; Habari na Mawasiliano; Fedha na Bima; Utawala na Ulinzi; Shughuli za Kitaaluma, Sayansi na Ufundi; Huduma zinazohusiana na Utawala; Upangishaji Majengo; Elimu, Afya, Sanaa na Burudani; Huduma nyingine za Kijamii; na Shughuli za Kaya katika Kuajiri) zilikuwa na mchango mkubwa zaidi wa asilimia 39.9 zikifuatiwa na shughuli za Msingi (Kilimo cha Mazao, Mifugo, Misitu, Uvuvi) asilimia 34.5 na shughuli za Kati (Uchimbaji Madini na Mawe; Viwanda, Umeme, Maji Safi na Majitaka; na Ujenzi) asilimia 25.6. Mchango wa shughuli kuu za kiuchumi katika Pato la Taifa umekokotolewa kwa bei za mwaka husika kabla ya kujumuisha kodi.

**Kielelezo Na. 4: Mchango katika Pato la Taifa kwa Bei za Miaka Inayohusika**





Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2022

### 1.5.3 Ukuaji wa Shughuli za Uchumi Robo ya Tatu, Mwaka 2022

Katika kipindi cha Julai hadi Septemba 2022, shughuli ya Habari na Mawasiliano iliongoza kwa ukuaji wa asilimia 13.7; ikifuatiwa na huduma za Chakula na Malazi (asilimia 13.2); Fedha na Bima (asilimia 12.0); Uchimbaji Madini na Mawe (asilimia 9.8); Umeme (asilimia 9.7) na Huduma Nyingine za Jamii zinazojumuisha Sanaa na Burudani na Shughuli za Kaya katika Kuajiri (asilimia 9.0).

**Kielelezo Na. 5: Viwango vya Ukuaji wa Shughuli za Uchumi, Robo ya Tatu, Mwaka 2022**




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2022

1. (Kumbuka: Huduma Nyingine za Kijamii zinajumuisha shughuli za Mashirika yasiyo ya Kiserikali yanayohudumia jamii, Vyama vya Siasa, Makanisa, Misikiti, Sanaa na Burudani na Shughuli za Kaya katika Kuajiri)

### 1.5.4 Mchango katika Kiwango cha Ukuaji Robo ya Tatu, Mwaka 2022

Shughuli zote za uchumi zilizofanyika katika kipindi cha Julai hadi Septemba 2022 zilichangia ukuaji wa uchumi kwa kiwango cha asilimia 5.2 ikilinganishwa na asilimia 5.5 kipindi kama hicho mwaka 2021. Shughuli za uchumi zilizokuwa na mchango mkubwa katika ukuaji wa asilimia 5.2 zilikuwa ni pamoja na: Uchukuzi na Uhifadhi Mzigo (asilimia 14.2); Kilimo (asilimia 12.4), Uchimbaji Madini na Mawe (asilimia 9.8); Ujenzi (asilimia 8.3), Fedha na Bima (asilimia 8.3); na Uzalishaji Viwandani (asilimia 7.9).

## 2.1 Ukuaji wa Uchumi kwa Shughuli za Kiuchumi

## 2.2 Kilimo, Misitu na Uvuvi


Shughuli hii inahusika na uvunaji wa rasilimali za asili za mboga za majani na wanyama. Shughuli hizi zinazojumuisha mazao ya kupandwa, ufugaji na uzalishaji wa wanyama, uvunaji wa miti na mimea mingine, wanyama au bidhaa za wanyama kutoka katika mashamba ya ufugaji au mazingira ya asili.

### 2.2.1 Mazao

Mazao makuu yaliyojumuishwa ni pamoja na mahindi, mpunga, ulezi/mtama, nafaka nyingine, mihogo, viazi mviringo, viazi vitamu, maharagwe, mikunde, mbegu za mafuta, mboga mboga, ndizi, matunda mengine, karanga, kahawa, pamba, chai, tumbaku na mazao mengine ya chakula na biashara.

Shughuli hii iliongezeka kwa kiwango kidogo cha asilimia 2.7 katika robo ya tatu ya mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 6.8 kipindi kama hicho mwaka 2021. Kasi ndogo ya ukuaji ilisababishwa na uzalishaji mdogo uliotokana kutokuwepo kwa mvua za kutosha katika kipindi cha Julai hadi Septemba 2022.

**Kielelezo Na. 6: Uzalishaji wa Baadhi ya Mazao, Robo ya Tatu Mwaka 2021 na 2022**




Chanzo: Wizara ya Kilimo, 2022

Mazao ambayo yalichangia katika ukuaji wa shughuli hii katika robo ya tatu ya mwaka 2022 ni pamoja na mihogo iliyoongezeka kwa asilimia 17.0 kutoka tani 254 elfu mwaka 2021 hadi tani 297 elfu mwaka 2022, ndizi ziliongezeka kwa asilimia 8.5 kutoka tani 135 elfu mwaka 2021 hadi tani 146 elfu mwaka 2022. Mazao mengine ni viazi vitamu vilivyoongezeka kwa asilimia 4.6 kutoka tani 108 elfu mwaka 2021 hadi tani 113 elfu mwaka 2022 na maharage na mazao jamii ya mikunde yaliyoongezeka kwa asilimia 1.3 kutoka tani 81 elfu mwaka 2021 hadi tani 82 elfu mwaka 2022.

### 2.2.2 Mifugo

Shughuli hii inahusika na ufugaji ng'ombe wa asili na wa kisasa; mbuzi, kondoo, punda, farasi, nguruwe, sungura, kuku wa kienyeji na kisasa; na ndege wa aina nyingine.

Katika robo ya tatu ya mwaka 2022, uzalishaji wa mifugo uliongezeka hadi asilimia 5.1 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2021. Ukuaji huo ulichangiwa na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa za mifugo, ukuaji wa miji pamoja na kuongezeka kwa uelewa wa wananchi juu ya umuhimu wa lishe bora.

### 2.2.3 Misitu

Shughuli hii inahusisha uzalishaji na uvunaji wa mazao ya misitu kama vile magogo, mkaa, kuni, matawi ya miti, na bidhaa nyingine zisizo za miti kama vile asali na nta.

Shughuli ya misitu ilikua kwa kiwango kidogo cha asilimia 3.0 katika robo ya tatu ya mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 6.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2021. Ukuaji huo ulitokana na kupungua kwa uvunaji wa bidhaa za misitu kwa kuzingatia usimamizi wa rasilimali za misitu na pia juhudi za Serikali kuhakikisha uvunaji endelevu wa bidhaa za misitu.

### 2.2.4 Uvuvi

Shughuli ya uvuvi inahusika na uvunaji wa rasilimali za uvuvi katika maji ya bahari na vyanzo vingine vya maji baridi.

Shughuli ya uvuvi ilikua kwa kiwango cha asilimia 0.9 katika robo ya tatu ya mwaka 2022 ikilinganishwa na kiwango hasi cha ukuaji wa asilimia 2.2 kipindi kama hicho mwaka 2021. Ukuaji wa shughuli ya uvuvi ulichangiwa na kuimarika kwa uzalishaji wa mazao ya uvuvi katika kipindi hicho.

## 2.3 Uchimbaji Madini na Mawe

Shughuli ya uchimbaji wa Madini na Mawe inahusisha uchimbaji au ukusanyaji wa madini katika hali zake za yabisi kama vile makaa ya mawe, vimiminika (petroli) au gesi (gesi asilia). Uchimbaji wa madini na mawe hufanyika chini ya ardhi, ukusanyaji juu ya ardhi au kwenye visima. Pia inajumuisha shughuli za ziada zinazolenga kutayarisha madini kwa ajili ya kuuzwa, kwa mfano, kusaga, kusafisha na kukausha. Shughuli hizi mara nyingi zinafanywa na vitengo ambavyo vinavuna rasilimali za madini / au nyingine zilizopo karibu na migodi.

Shughuli ya uchimbaji wa madini na mawe imegawanyika katika maeneo makuu manne ambayo ni:

1) Madini ya makaa ya mawe;
2) Petroli na gesi asilia;
3) Uchimbaji wa madini ya chuma; na
4) Madini ya kokoto na mawe.

Kiwango cha ukuaji wa shughuli ya uchimbaji wa madini na mawe kiliongezeka kwa asilimia 9.8 katika robo ya tatu ya mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 13.1

kipindi kama hicho mwaka 2021. Kiwango cha ukuaji kilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa madini ya dhahabu, almasi, chumvi, makaa ya mawe na gesi asilia.

Katika kipindi hicho, uzalishaji wa baadhi ya madini uliongezeka kama ifuatavyo: dhahabu iliongezeka hadi kilo 17,516 mwaka 2022 kutoka 14,915 mwaka 2021, almasi iliongezeka hadi karati 74,462 mwaka 2022 kutoka karati 19,418 kipindi kama hicho mwaka 2021 na makaa ya mawe yaliongezeka hadi tani 774,398 mwaka 2022 kutoka tani 191,607 katika kipindi hicho mwaka 2021.

**Jedwali Na. 1: Uzalishaji wa Madini, Robo ya Tatu Mwaka 2016 – 2022**

| Madini | Kipimo | 2017 | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Dhahabu | Kg | 11,165 | 10,144 | 12,276 | 13,698 | 14,915 | 17,516 |
| Makaa ya Mawe | Tani | 137,320 | 193,240 | 131,705 | 183,734 | 191,607 | 774,398 |
| Chumvi | Tani | 13,380 | 38,296 | 22,027 | 20,853 | 26,556 | 73,566 |
| Gesi Asilia | Mita za Ujazo Milioni | 14,119 | 15,721 | 16,836 | 14,029 | 15,775 | 20,250 |
| Almasi | Karati | 88,943 | 80,509 | 56,682 | 35,243 | 19,418 | 74,462 |

Chanzo: Wizara ya Madini, 2022

## 2.4 Uzalishaji Viwandani

Shughuli ya uzalishaji viwandani inahusisha uchakataji wa bidhaa kutoka katika hali yake ya kawaida na kuzalisha bidhaa za aina nyingine ambazo zinaweza kutumika moja kwa moja na mlaji wa mwisho au kutumika kuzalisha bidhaa nyingine. Bidhaa zinazoweza kuchakatwa ni pamoja na bidhaa za kilimo, misitu, uvuvi, madini na bidhaa nyingine za viwandani.

Kiwango cha ukuaji wa shughuli ya uzalishaji viwandani kiliongezeka hadi asilimia 4.5 katika robo ya tatu mwaka 2022 kutoka asilimia 3.9 kipindi kama hicho mwaka 2021. Ukuaji huu ulichangiwa na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa za viwandani.

## 2.5 Umeme

Shughuli hii inahusika na uzalishaji na usambazaji wa umeme na gesi asilia kupitia miundombinu ya kudumu ya waya na mabomba. Uzalishaji wa umeme ni kutoka katika vyanzo vya maji, mafuta na gesi. Shughuli hii pia inahusika na usambazaji wa umeme. Vyanzo vikuu vya takwimu za uzalishaji wa umeme ni kutoka katika makampuni ya uzalishaji wa umeme.

Ukuaji wa shughuli ya uzalishaji wa umeme hutegemea kiasi cha umeme kilichozalishwa na kusambazwa kwa wateja mbalimbali wa nishati ya umeme. Katika robo ya tatu ya mwaka 2022, umeme uliosambazwa kwa wateja uliongezeka hadi saa za kilowati milioni 1,983 kutoka saa za kilowati milioni 1,807 kipindi kama hicho mwaka 2021.

Shughuli ya uzalishaji umeme ilikua kwa kwa kiwango cha asilimia 9.7 katika robo ya tatu ya mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 10.0 kipindi kama hicho mwaka 2021.

### 2.6 Maji

Shughuli hii inahusika na kukusanya na kusafisha maji kwa ajili ya ugavi wa maji, kusafisha maji ya bahari kwa kuondoa chumvi ili kuweza kuzalisha maji ya kutumia kama bidhaa kuu na kukusanya maji moja kwa moja kutoka katika visima kwa ajili ya matumizi ya makampuni ya maji au matumizi binafsi katika kilimo au kaya. Vilevile, shughuli hii inahusika na ukusanyaji wa maji taka.

Kiashiria cha kuongezeka kwa kiwango cha ukuaji wa shughuli ya usambazaji maji ni kiasi cha maji kilichozalishwa. Katika robo ya tatu ya mwaka 2022, kiasi cha maji kilichozalishwa kilikuwa mita za ujazo milioni 97.3 ukilingaisha na mita za ujazo milioni 97.5 kipindi kama hicho mwaka 2021.

Kiwango cha ukuaji wa shughuli ya usambazaji maji kiliongezeka kwa kiwango kidogo cha asilimia 0.1 katika robo ya tatu ya mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 4.5 kipindi kama hicho mwaka 2021. Sababu zilisababisha ongezeko dogo ni pamoja na kupungua kwa uzalishaji wa maji katika kipindi hicho.

### 2.7 Ujenzi

Shughuli hii inajumuisha ujenzi wa aina zote na shughuli maalum za ujenzi kwa ajili ya majengo na kazi za uhandisi. Shughuli hii inajumuisha pia ujenzi mpya, ukarabati, kufanya mabadiliko makubwa kwenye majengo na ujenzi wa miundombinu.

Aidha, shughuli hizi zinajumuisha ujenzi wa nyumba za kuishi/makazi, majengo ya biashara/ofisi, maduka na majengo mengine ya umma na miundombinu ya mashambani. Ujenzi pia unajumuisha ujenzi wa barabara, madaraja, reli, viwanja vya ndege, bandari na miundombinu ya maji, mifumo ya umwagiliaji, mifumo ya

majitaka, miundombinu ya viwanda, mabomba, mifumo ya umeme na vituo vya michezo.

Shughuli ya ujenzi iliongezeka kwa kiwango kidogo cha cha asilimia 2.7 katika robo ya tatu ya mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 5.8 ya kipindi kama hicho mwaka 2021. Tathmini ya ukuaji wa shughuli ya ujenzi hutumia viashiria vya uzalishaji wa bidhaa za ndani ya nchi zinazotumika katika shughuli za ujenzi. Ongezeko dogo la uzalishaji wa bidhaa hizo ambazo ni pamoja na chuma zilichangia ukuaji huo.

## 2.8 Biashara na Matengenezo

Shughuli hii inajumuisha uuzaji wa jumla na rejareja (uuzaji wa bidhaa bila ya kufanya mabadiliko) wa aina yoyote ya bidhaa, pamoja na utoaji wa huduma kwa ajili ya uuzaji wa bidhaa. Pia inahusisha ukarabati wa magari na usimikaji wa mitambo na ukarabati wa bidhaa za binafsi na za nyumbani. Shughuli kuu ni kununua na kuuza bidhaa.

Ukuaji wa shughuli za Biashara na Matengenezo ziliongezeka hadi asilimia 3.9 katika robo ya tatu ya mwaka 2022 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 1.9 kipindi kama hicho mwaka 2021. Ukuaji wa shughuli hii ulichangiwa na kuongezeka kwa bidhaa zilizouzwa ikiwa ni pamoja na bidhaa za kilimo, bidhaa zilizozalishwa viwandani na zilizoagizwa kutoka nje ya nchi.

## 2.9 Uchukuzi na Uhifadhi wa Mizigo

Shughuli hii inahusisha utoaji wa huduma ya usafiri wa abiria au/na mizigo, ikiwa ni kwa ratiba maalum au isiyokuwa na ratiba, kwa njia ya reli, bomba, barabara, maji au anga na shughuli zinazohusiana ikiwa ni pamoja na utunzaji wa mizigo na uhifadhi. Shughuli hii pia inajumuisha kukodisha vifaa vya usafiri na madereva na shughuli za posta na usafirishaji wa vifurushi.

Kasi ya ukuaji wa shughuli ya Uchukuzi na Uhifadhi wa Mizigo iliongezeka kwa hadi asilimia 9.4 katika robo ya tatu ya mwaka 2022 kutoka kiwango hasi cha ukuaji wa asilimia 0.6 kipindi kama hicho mwaka 2021. Ukuaji ulitokana na kuongezeka kwa idadi ya abiria na mizigo iliyosafirishwa kwa njia ya barabara katika kipindi hicho.

## 2.10 Huduma ya Malazi na Chakula

Shughuli hii inajumuisha utoaji huduma ya makazi ya muda mfupi kwa wageni na wasafiri wengine na utoaji wa huduma ya chakula na vinywaji kwa mlaji wa mwisho.

Shughuli ya Malazi na Chakula iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 13.2 katika robo ya tatu ya mwaka 2022 ikilinganishwa na kiwango cha asilimia 14.3 kipindi kama hicho mwaka 2021. Kasi ya ukuaji wa shughuli ya malazi na huduma za chakula ilichangiwa na kuongezeka kwa mahitaji ya huduma za utalii kutokana na idadi kubwa ya watalii waliongia nchini kwa kipindi husika. Watalii waliongia nchini katika kipindi cha Julai hadi Septemba 2022 iliongezeka hadi watalii 458,783 kutoka watalii 249,437 mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia 83.9.

## 2.11 Habari na Mawasiliano

Shughuli hii inahusika na uchapishaji, upigaji picha za kawaida, picha za video na uzalishaji wa programu za televisheni, kurekodi sauti na kuchapisha muziki, shughuli za programu na utangazaji kwa mfano utangazaji wa redio na televisheni, mawasiliano ya simu, programu za kompyuta, ushauri na shughuli zinazohusiana na shughuli za huduma za habari kama vile uchakataji wa taarifa.

Kiwango cha ukuaji wa shughuli ya Habari na Mawasiliano kiliongezeka hadi asilimia 13.7 katika robo ya tatu ya mwaka 2022 kutoka asilimia 8.3 kipindi kama hicho mwaka 2021. Kasi ya ukuaji ilichangiwa na kuongezeka kwa muda wa maongezi, huduma za ujumbe mfupi uliotumwa na kuongezeka kwa idadi ya wateja waliopata huduma za fedha kupitia mitandao ya simu pamoja na huduma za utangazaji na huduma za inteneti kwa ujumla.

**Jedwali Na. 2: Viashiria vya Huduma za Mawasiliano, Robo ya Tatu Mwaka 2020 – 2022**

| Kiashiria, kwa Robo Mwaka | 2020 | 2021 | 2022 |
|---|---|---|---|
| Muda wa maongezi (dakika milioni) | 21,966 | 25,203 | 33,374 |
| Ujumbe Mfupi uliotumwa (milioni) | 31,758 | 35,605 | 40,211 |
| Wateja wa huduma za fedha mitandao ya simu, idadi (‘000’) mwisho wa mwezi Juni | 30,587 | 33,155 | 39,591 |


Chanzo: Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, 2022

## 2.12 Fedha na Bima

Shughuli hii inahusika na utoaji wa huduma za fedha, bima, pensheni ya hiari, na huduma nyingine za fedha.

Huduma za Fedha na Bima ziliongezeka hadi asilimia 12.0 katika robo ya tatu ya mwaka 2022 kutoka asilimia 4.8 katika robo ya tatu ya mwaka 2021. Ukuaji wa shughuli za Fedha na Bima zilichangiwa na kuongezeka kwa asilimia 18.0 kwa amana kutoka shilingi trilioni 25.0 mwaka 2021 hadi shilingi trilioni 29.5 mwaka 2022; ongezeko la asilimia 21.9 la mikopo kutoka shilingi trilioni 20.8 mwaka 2021 hadi shilingi trilioni 25.4 mwaka 2022; na pia kuongezeka kwa kiwango cha ukuaji hadi asilimia 5.0 wa shughuli za Bima mwaka 2022 kutoka asilimia 1.5 kipindi kama hicho mwaka 2021.

**Kielelezo Na. 7: Jumla ya Mikopo na Amana (Sh. Trilioni), Robo ya Tatu Mwaka 2017 – 2022**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania, 2022

## 2.13 Upangishaji Majengo

Shughuli hii inahusika na utoaji wa huduma za kuuza au kununua majengo, kukodisha mali, majengo na pia kutoa huduma nyingine za mali isiyohamishika ikiwa ni pamoja na kupima mali isiyohamishika kama vile viwanja.

Kiwango cha ukuaji wa shughuli ya Upangishaji Majengo kiliongezeka kwa asilimia 4.4 katika robo ya tatu mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 4.6 kipindi kama hicho mwaka 2021. Ongezeko la mahitaji ya huduma za malazi hususan katika maeneo ya mjini lilichangia ukuaji wa shughuli hii ya uchumi.

## 2.14 Shughuli za Kitaalam, Ufundi na Sayansi

Shughuli hii inajumuisha shughuli maalum za kitalaam, kisayansi na kiufundi. Shughuli hizi zinahitaji kiwango cha juu cha mafunzo, pamoja na kupata ujuzi maalum unaotumika kutoa huduma kwa watumiaji. Shughuli hii inahusisha huduma za kisheria na uhasibu; ushauri na usimamizi; usanifu na uhandisi; kupima na uchambuzi wa kitaalam; utafiti wa kisayansi na maendeleo; matangazo na utafiti wa masoko; utaalam wa aina nyingine wa kisayansi na kiufundi pamoja na shughuli za ugani.

Kasi ya ukuaji wa shughuli za Kitaalam, Kisanyansi na Kiufundi iliongezeka hadi asilimia 6.8 katika robo ya tatu ya mwaka 2022 kutoka asilimia 5.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2021. Kuongezeka kwa huduma za kisheria na uhasibu katika shughuli hii ya uchumi kulichangia kiwango cha ukuaji uliofikiwa.

## 2.15 Huduma Zinazohusiana na Utawala

Shughuli hii inajumuisha huduma mbalimbali zinazosaidia kufanyika kwa biashara ambazo ni huduma za: kukodisha vifaa, ajira, uwakala wa kampuni za usafiri, kuongoza watalii, kuandaa malazi; na huduma nyingine zinazohusiana na usalama na uchunguzi; pamoja na huduma kwenye majengo na uboreshaji wa mazingira.

Kiwango cha ukuaji wa Huduma zinazohusiana na Utawala kiliongezeka kwa asilimia 3.6 katika robo ya tatu ya mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 6.0 kipindi kama hicho mwaka 2021. Kuongezeka kwa huduma za uwakala wa usafiri wa watalii ulichangia zaidi ukuaji wa shughuli hii.

## 2.16 Utawala na Ulinzi

Shughuli ya Utawala na Ulinzi inahusika na kutunga na kutafsiri sheria, kukusanya kodi, ulinzi wa mipaka ya nchi, usalama wa raia na mali zao, huduma za uhamiaji, pamoja na uendeshaji wa shughuli za Serikali kwa ujumla. Aidha, huduma za mifuko ya hifadhi ya jamii ya lazima imejumuishwa katika shughuli ya Utawala na Ulinzi.

Ukuaji wa shughuli ya Utawala na Ulinzi uliimarika zaidi hadi asilimia 6.9 katika robo ya tatu ya mwaka 2022 kutoka asilima 6.6 kipindi kama hicho mwaka 2021. Kasi ya ukuaji ilitokana na ongezeko la matumizi ya fedha za Serikali katika utoaji wa huduma za jamii, ongezeko la mishahara, kulipa malimbikizo ya madai ya

wafanyakazi na utekelezaji wa kazi za ulinzi na usalama pamoja na uendeshaji wa Serikali kwa ujumla.

### 2.17 Elimu

Shughuli hii inajumuisha utoaji wa elimu katika ngazi zote, kwa njia ya kuongea au maandishi au kwa njia ya redio na televisheni au njia nyingine za mawasiliano. Vilevile, inajumuisha elimu inayotolewa na taasisi mbalimbali katika mfumo wa kawaida wa shule katika ngazi tofauti pamoja na elimu ya watu wazima na elimu ya kujifunza kusoma na kuandika. Shughuli hii inajumuisha elimu katika sekta ya umma na binafsi.

Shughuli ya Elimu iliongezeka hadi asilimia 6.5 katika robo ya tatu ya mwaka 2022 kutoka asilimia 6.2 katika kipindi kama hicho mwaka 2021. Ukuaji wa shughuli hii umetokana na kuongezeka kwa udahili wa wanafunzi katika shule za msingi, sekondari na vyuo vya elimu ya juu vya umma na binafsi. Aidha, kuongezeka kwa mishahara na matumizi ya Serikali katika utoaji wa elimu bila ada kulichangia ukuaji wa shughuli hii.

### 2.18 Afya

Shughuli hii inajumuisha utoaji wa huduma za afya na maendeleo ya jamii. Inajumuisha pia huduma za afya zinazotolewa na wataalam wa matibabu katika hospitali na vituo vingine, shughuli nyingine za huduma za makazi ambazo zinahusisha shughuli za huduma za afya kwa jamii bila ushirikishwaji wa wataalam wa huduma za afya.

Shughuli ya utaoji wa huduma za afya iliongezeka hadi asilimia 7.3 katika robo ya tatu ya mwaka 2022 kutoka asilimia 7.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2021. Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa mishahara ya watumishi wa umaa katika sekta hii pamoja na kuendelea kuboreshwa kwa huduma za utoaji wa huduma za afya kwa jamii katika ngazi zote za kutolea huduma.

### 2.19 Huduma Nyingine za Jamii

Shughuli hii inajumuisha shughuli za mashirika ya uanachama, ukarabati wa vifaa vya kieletroniki na bidhaa za kibinafsi za nyumbani na shughuli mbalimbali za huduma za binafsi ambazo hazijumuishwi kwenye shughuli nyingine. Pia inajumuisha shughuli ya Sanaa na Burudani na shughuli za kaya katika kuajiri.

Kasi ya ukuaji wa shughuli ya Huduma Nyingine za Jamii iliongezeka kwa asilimia 9.0 katika robo ya tatu ya mwaka 2022 ikilinganishwa na asilimia 12.1 kipindi kama hicho mwaka 2021. Ongezeko la watalii, idadi ya watu katika maeneo ya mjini na mahitaji ya huduma za jamii lilichangia ukuaji wa shughuli hii ya uchumi.

## 3.0 Hitimisho

Katika robo ya tatu mwaka 2022, Pato Halisi la Taifa (kwa bei za mwaka kizio 2015) liliongezeka kwa kiwango cha asilimia 5.2 ikilinganishwa na asilimia 5.5 kipindi kama hicho mwaka 2021. Shughuli za uchumi zilizokuwa na kiwango kikubwa cha ukuaji zilikuwa ni pamoja na: Habari na Mawasiliano (asilimia 13.7); Chakula na Malazi (asilimia 13.2); Fedha na Bima (asilimia 12.0); Uchimbaji Madini na Mawe (asilimia 9.8); na Umeme (asilimia 9.7).

**Kiambatisho Na. 1: Pato la Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi kwa Bei za Mwaka wa Kizio 2015 – Sh. Milioni**

| Mwaka | Nusu Mwaka | kilimo | Madini na Mawe | Viwanda | Umeme | Maji safi na maji taka | Ujenzi | Biashara na Matengenezo | Malazi na Huduma ya Chakula | Uchukuzi na Uhifadhi Mizigo | Habari na Mawasiliano | Fedha na Bima |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2012 | | 21,807,030 | 3,314,742 | 6,066,989 | 669,069 | 358,361 | 7,578,263 | 7,371,411 | 1,343,924 | 5,710,466 | 1,266,747 | 3,444,161 |
| 2013 | | 22,408,192 | 3,464,721 | 6,292,514 | 723,608 | 367,890 | 9,023,353 | 7,682,286 | 1,356,204 | 6,050,976 | 1,414,116 | 3,405,940 |
| 2014 | | 23,952,077 | 3,687,273 | 6,919,794 | 815,297 | 381,760 | 9,253,082 | 8,444,243 | 1,397,782 | 6,577,706 | 1,560,064 | 3,764,113 |
| 2015 | | 25,234,560 | 4,055,619 | 7,411,672 | 798,801 | 390,758 | 10,446,797 | 8,747,862 | 1,421,916 | 6,929,895 | 1,681,098 | 4,189,021 |
| 2016 | | 26,436,338 | 4,356,709 | 8,213,364 | 869,262 | 417,899 | 11,960,720 | 9,260,703 | 1,480,052 | 7,324,856 | 1,718,548 | 4,235,515 |
| 2017 | | 28,008,976 | 4,588,624 | 8,889,818 | 877,667 | 444,660 | 13,765,005 | 9,821,248 | 1,525,619 | 7,815,845 | 1,824,471 | 4,115,393 |
| 2018 | | 29,504,198 | 4,659,195 | 9,623,501 | 928,174 | 477,510 | 15,655,747 | 10,396,691 | 1,604,391 | 8,736,561 | 1,989,717 | 4,094,972 |
| 2019 | | 30,802,027 | 5,485,112 | 10,184,558 | 994,879 | 510,411 | 17,802,021 | 10,965,038 | 1,645,950 | 9,493,191 | 2,133,312 | 4,281,167 |
| 2020 | | 32,323,876 | 5,878,342 | 10,646,279 | 1,049,610 | 540,159 | 19,421,672 | 11,196,339 | 1,419,654 | 10,293,276 | 2,313,029 | 4,412,967 |
| 2021 | | 33,577,189 | 6,442,881 | 11,155,762 | 1,154,204 | 575,213 | 20,256,410 | 11,590,493 | 1,514,711 | 10,658,344 | 2,524,564 | 4,629,490 |
| | | | | | | | | | | | | |
| 2012 | 1 | 5,972,854 | 845,470 | 1,528,195 | 151,473 | 86,422 | 1,816,993 | 1,877,418 | 321,003 | 1,208,445 | 281,981 | 849,590 |
| | 2 | 5,182,996 | 825,383 | 1,544,666 | 164,427 | 89,319 | 1,808,760 | 1,855,404 | 320,427 | 1,456,176 | 303,507 | 844,631 |
| | 3 | 4,092,001 | 833,592 | 1,499,895 | 172,946 | 92,526 | 2,012,312 | 1,725,714 | 358,248 | 1,489,645 | 327,526 | 886,247 |
| | 4 | 6,559,178 | 810,297 | 1,494,233 | 180,223 | 90,094 | 1,940,197 | 1,912,875 | 344,245 | 1,556,199 | 353,733 | 863,692 |
| 2013 | 1 | 5,994,220 | 748,412 | 1,459,422 | 167,460 | 87,306 | 2,146,785 | 1,828,162 | 332,454 | 1,519,508 | 312,238 | 811,387 |
| | 2 | 5,376,452 | 850,463 | 1,547,040 | 177,004 | 90,069 | 2,111,891 | 1,884,307 | 324,659 | 1,501,581 | 343,060 | 836,571 |
| | 3 | 4,199,755 | 875,290 | 1,677,731 | 181,477 | 85,918 | 2,389,873 | 1,893,295 | 354,104 | 1,513,039 | 358,452 | 881,698 |
| | 4 | 6,837,765 | 990,556 | 1,608,322 | 197,667 | 104,598 | 2,374,804 | 2,076,522 | 344,987 | 1,516,849 | 400,366 | 876,284 |
| | | | | | | | | | | | | |
| 2014 | 1 | 6,335,448 | 937,448 | 1,621,405 | 201,849 | 87,893 | 2,182,230 | 2,054,479 | 346,623 | 1,625,429 | 342,909 | 912,095 |
| | 2 | 5,877,120 | 871,899 | 1,706,772 | 182,845 | 94,708 | 2,507,336 | 2,073,942 | 339,327 | 1,616,710 | 380,305 | 927,895 |
| | 3 | 4,450,294 | 929,381 | 1,788,128 | 213,998 | 97,099 | 2,228,708 | 2,035,245 | 361,470 | 1,686,150 | 414,058 | 960,721 |
| | 4 | 7,289,215 | 948,546 | 1,803,489 | 216,605 | 102,059 | 2,334,808 | 2,280,578 | 350,362 | 1,649,417 | 422,793 | 963,401 |
| | | | | | | | | | | | | |
| 2015 | 1 | 6,605,887 | 923,326 | 1,733,636 | 211,828 | 96,862 | 2,438,046 | 2,093,973 | 346,778 | 1,654,599 | 386,446 | 995,846 |
| | 2 | 6,347,239 | 965,335 | 1,820,111 | 199,281 | 92,862 | 2,690,105 | 2,195,254 | 345,054 | 1,676,064 | 412,841 | 1,011,653 |
| | 3 | 4,656,388 | 960,427 | 1,939,664 | 192,215 | 99,585 | 2,601,253 | 2,162,776 | 372,080 | 1,764,202 | 441,478 | 1,076,143 |
| | 4 | 7,625,045 | 1,206,532 | 1,918,260 | 195,477 | 101,448 | 2,717,393 | 2,295,860 | 358,003 | 1,835,030 | 440,334 | 1,105,380 |
| | | | | | | | | | | | | |
| 2016 | 1 | 6,788,342 | 1,017,609 | 1,965,656 | 214,850 | 95,779 | 2,859,933 | 2,295,506 | 358,142 | 1,818,390 | 401,047 | 1,111,056 |
| | 2 | 6,853,095 | 1,109,064 | 1,996,019 | 210,034 | 100,816 | 2,995,869 | 2,318,553 | 347,167 | 1,819,827 | 421,552 | 1,052,954 |
| | 3 | 4,936,684 | 1,098,979 | 2,080,908 | 214,673 | 103,584 | 3,208,669 | 2,300,383 | 385,323 | 1,854,653 | 451,160 | 1,053,955 |
| | 4 | 7,858,218 | 1,131,055 | 2,170,783 | 229,706 | 117,720 | 2,896,249 | 2,346,262 | 389,420 | 1,831,986 | 444,789 | 1,017,550 |
| | | | | | | | | | | | | |
| 2017 | 1 | 7,233,097 | 1,118,373 | 2,067,899 | 223,751 | 97,295 | 3,204,078 | 2,338,470 | 374,854 | 1,914,669 | 452,123 | 1,046,585 |
| | 2 | 7,283,729 | 1,057,691 | 2,187,504 | 207,413 | 105,045 | 3,631,267 | 2,437,212 | 359,355 | 1,910,951 | 449,234 | 1,028,221 |
| | 3 | 5,139,926 | 1,144,597 | 2,365,766 | 222,988 | 113,969 | 3,198,026 | 2,434,360 | 395,146 | 1,982,315 | 459,555 | 997,959 |
| | 4 | 8,352,224 | 1,267,964 | 2,268,650 | 223,515 | 128,352 | 3,731,635 | 2,611,207 | 396,263 | 2,007,909 | 463,560 | 1,042,628 |
| | | | | | | | | | | | | |
| 2018 | 1 | 7,718,169 | 1,054,655 | 2,173,169 | 225,002 | 100,913 | 3,703,467 | 2,437,093 | 391,664 | 2,082,426 | 522,202 | 1,017,158 |
| | 2 | 7,716,746 | 1,129,287 | 2,259,893 | 221,000 | 111,470 | 3,846,566 | 2,529,440 | 383,333 | 2,169,733 | 506,990 | 1,004,545 |
| | 3 | 5,333,826 | 1,166,716 | 2,530,756 | 235,534 | 126,137 | 3,711,275 | 2,601,411 | 425,407 | 2,222,813 | 481,219 | 1,036,270 |
| | 4 | 8,735,457 | 1,308,537 | 2,659,683 | 246,639 | 138,991 | 4,394,440 | 2,828,746 | 403,987 | 2,261,589 | 479,306 | 1,037,000 |
| | | | | | | | | | | | | |
| 2019 | 1 | 8,136,363 | 1,159,804 | 2,280,570 | 249,013 | 108,984 | 4,201,084 | 2,528,805 | 390,255 | 2,312,794 | 563,479 | 1,069,571 |
| | 2 | 8,037,085 | 1,323,857 | 2,384,031 | 239,855 | 118,551 | 4,636,133 | 2,673,436 | 393,345 | 2,322,004 | 538,430 | 1,046,930 |
| | 3 | 5,485,957 | 1,413,025 | 2,749,036 | 247,875 | 139,826 | 4,350,024 | 2,794,035 | 442,538 | 2,407,844 | 516,796 | 1,084,937 |
| | 4 | 9,142,621 | 1,588,425 | 2,770,921 | 258,136 | 143,049 | 4,614,781 | 2,968,762 | 419,812 | 2,450,548 | 514,606 | 1,079,730 |
| | | | | | | | | | | | | |
| 2020 | 1 | 8,469,003 | 1,365,988 | 2,387,165 | 264,424 | 116,821 | 4,408,146 | 2,650,981 | 400,323 | 2,505,607 | 610,395 | 1,114,722 |
| | 2 | 8,366,922 | 1,438,625 | 2,479,030 | 247,858 | 124,044 | 5,203,762 | 2,668,493 | 330,902 | 2,541,456 | 592,499 | 1,078,981 |
| | 3 | 5,838,125 | 1,482,857 | 2,882,547 | 258,781 | 150,811 | 4,955,258 | 2,851,918 | 331,271 | 2,576,818 | 560,949 | 1,105,924 |
| | 4 | 9,649,826 | 1,590,872 | 2,897,536 | 278,547 | 148,483 | 4,854,506 | 3,024,946 | 357,157 | 2,669,394 | 549,186 | 1,113,341 |
| | | | | | | | | | | | | |
| 2021 | 1 | 8,684,485 | 1,489,458 | 2,532,535 | 283,588 | 127,311 | 4,641,094 | 2,768,552 | 374,418 | 2,730,301 | 661,347 | 1,144,304 |
| | 2 | 8,585,645 | 1,574,503 | 2,589,415 | 277,917 | 134,491 | 5,302,015 | 2,783,463 | 364,386 | 2,666,798 | 659,757 | 1,119,611 |
| | 3 | 6,139,356 | 1,677,259 | 2,995,394 | 284,691 | 157,663 | 5,241,139 | 2,905,293 | 378,526 | 2,560,195 | 607,521 | 1,158,549 |
| | 4 | 10,167,704 | 1,701,661 | 3,038,419 | 308,008 | 155,747 | 5,072,162 | 3,133,185 | 397,381 | 2,701,050 | 595,938 | 1,207,026 |
| | | | | | | | | | | | | |
| 2022 | 1 | 9,034,897 | 1,616,392 | 2,692,630 | 307,061 | 142,426 | 4,893,120 | 2,918,220 | 379,909 | 2,775,741 | 714,257 | 1,260,182 |
| | 2 | 8,826,067 | 1,665,101 | 2,711,874 | 302,148 | 147,326 | 5,512,600 | 2,910,376 | 411,599 | 2,802,643 | 720,203 | 1,230,716 |
| | 3 | 6,348,759 | 1,841,754 | 3,128,705 | 312,393 | 157,751 | 5,381,177 | 3,018,560 | 428,373 | 2,799,725 | 691,002 | 1,297,825 |
| | 4 | | | | | | | | | | | |

**Kiambatisho Na. 1 (Kinaendela.): Pato la Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi kwa Bei za Mwaka wa Kizio 2015 – Sh. Milioni**

| Mwaka | Nusu mwaka | Utawala na Ulinzi | Sughuli za kitaaluma, Sayansi na Ufundi | Huduma zinazohusiana na Utawala | Upangishaji Majengo | Elimu | Afya na Huduma za Jami | Huduma nyingine za Kijamii | Jumla ya Ongezeko la Thamani | Ongeza kodi katika bidhaa | Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2012 | | 3,623,123 | 322,260 | 1,417,467 | 2,606,439 | 1,922,643 | 1,284,594 | 910,388 | 71,018,076 | 6,961,771 | 77,979,847 |
| 2013 | | 3,974,206 | 385,090 | 1,660,994 | 2,714,775 | 1,927,633 | 1,245,030 | 991,460 | 75,088,988 | 8,179,129 | 83,268,117 |
| 2014 | | 4,242,164 | 447,921 | 1,976,260 | 2,828,970 | 2,186,260 | 1,349,941 | 1,088,317 | 80,873,021 | 8,001,090 | 88,874,111 |
| 2015 | | 4,548,604 | 518,123 | 2,183,917 | 2,949,598 | 2,413,306 | 1,419,090 | 1,144,099 | 86,484,736 | 7,864,579 | 94,349,316 |
| 2016 | | 4,793,820 | 606,207 | 2,611,498 | 3,077,086 | 2,665,336 | 1,497,896 | 1,278,046 | 92,803,857 | 8,024,535 | 100,828,393 |
| 2017 | | 4,907,113 | 694,291 | 2,892,463 | 3,211,895 | 2,859,171 | 1,611,999 | 1,409,504 | 99,263,761 | 8,393,644 | 107,657,405 |
| 2018 | | 5,064,968 | 763,332 | 3,054,288 | 3,354,518 | 3,046,789 | 1,746,731 | 1,516,831 | 106,218,115 | 8,923,215 | 115,141,329 |
| 2019 | | 5,238,491 | 821,636 | 3,311,753 | 3,505,485 | 3,257,406 | 1,833,514 | 1,627,511 | 113,893,462 | 9,303,274 | 123,196,736 |
| 2020 | | 5,438,146 | 881,833 | 3,569,800 | 3,663,972 | 3,365,355 | 1,953,479 | 1,668,877 | 120,036,665 | 9,093,517 | 129,130,182 |
| 2021 | | 5,714,547 | 942,013 | 3,817,047 | 3,827,460 | 3,538,281 | 2,065,677 | 1,840,290 | 125,824,576 | 9,693,237 | 135,517,813 |
| | | | | | | | | | | | |
| 2012 | 1 | 803,642 | 74,831 | 340,487 | 641,698 | 461,652 | 309,228 | 217,530 | 17,788,914 | 1,732,167 | 19,521,081 |
| | 2 | 817,057 | 78,603 | 347,905 | 648,276 | 447,191 | 320,506 | 221,443 | 17,276,676 | 1,596,603 | 18,873,279 |
| | 3 | 976,077 | 82,451 | 358,076 | 654,899 | 505,099 | 339,618 | 234,892 | 16,641,764 | 1,737,034 | 18,378,797 |
| | 4 | 1,026,348 | 86,375 | 371,000 | 661,566 | 508,702 | 315,242 | 236,523 | 19,310,723 | 1,895,967 | 21,206,689 |
| 2013 | 1 | 897,436 | 90,376 | 386,679 | 668,325 | 454,979 | 299,454 | 239,370 | 18,443,971 | 1,947,582 | 20,391,553 |
| | 2 | 945,222 | 94,335 | 404,378 | 675,175 | 462,904 | 314,552 | 240,745 | 18,180,405 | 1,975,657 | 20,156,062 |
| | 3 | 1,061,729 | 98,252 | 424,098 | 682,119 | 501,425 | 323,848 | 253,497 | 17,755,599 | 2,088,269 | 19,843,868 |
| | 4 | 1,069,818 | 102,128 | 445,840 | 689,157 | 508,325 | 307,176 | 257,849 | 20,709,012 | 2,167,622 | 22,876,634 |
| | | | | | | | | | | | |
| 2014 | 1 | 1,007,519 | 105,963 | 469,602 | 696,292 | 510,028 | 322,658 | 266,230 | 20,026,099 | 2,102,819 | 22,128,918 |
| | 2 | 1,022,325 | 109,904 | 488,892 | 703,526 | 525,815 | 342,267 | 268,409 | 20,039,997 | 1,866,580 | 21,906,577 |
